## Nishani ya Uwakili

Mambo ya kuzingatia

1. Maana ya Uwakili wa Kikristo
2. Nyanja za Uwakili wa Kikristo
3. Uwezo wa kupanga ratiba yenye saa 24, ikionesha mpangilio wa mambo au kazi zako
4. Kufahamu na kuelewa kanuni muhimu za utendaji kazi
5. Kufahamu kanuni 12 za uwakili wa Kikristo
6. Kuelewa jinsi ya Kupangilia matumizi ya fedha unazopata
7. Kuwa na uwezo kueleza maana ya zaka na sadaka, jinsi zinavyotakiwa kutolewa na kupatikana kwake
8. Kuelewa talanta.

## Uwakili wa Kikristo

Ni mtindo wa Maisha ya mtu ambaye amemkubali Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake.

- Ni maisha ya mkiristo anayeongozwa na mapenzi ya MUNGU kwa maisha yote

**MAHUSIANO KATIKA UWAKILI**

1. Mahusiano kati ya MUNGU Muumbaji na mwanadamu
2. Uhusiano kati ya mtu na mwenzake
3. Mahusiano kati ya Mkiristo na mali aliyonayo na yote yanayomzunguka

**NYANJA ZA UWAKILI**

Kuna Nyanja kuu 6 za uwakili, tutajifunza 4

1. Uwakili wa Mwili
2. Uwakili wa Muda
3. Uwakili wa Talanta

4. Uwakili wa Mali

**ZAKA NA SADAKA**

**Zaka**:

- Zaka ni sehemu ya moja ya kumi ya mapato yanayopatikana kutokana na kazi iliyofanyika na kupata kipato/mshahara
- Zaka hutolewa kwa kuhesabiwa. Mfano fedha, mazao, wanyama n.k
- Zaka inaonesha utii
- Zaka inarudishwa
- Zaka inapotolewa inatangaza kwamba MUNGU PEKEE ndiye MUUMBAJI na MRUZUKU wa kila kitu. Zaburi 24:1, Ufunuo 14:6

**SADAKA**

- Sadaka ni sehemu ya pili katika mapato yangu kumshukuru MUNGU. Inaweza kutolewa zaidi ya zaka
- Sadaka ni shukrani kwa MUNGU.
- Sadaka inachaguliwa miongoni mwa alivyokubaliki MUNGU. Marko 41: 42-44
- Huchaguliwa inayofaa. Sadaka kilema haikubaliki kwa MUNGU. Malaki 1:6
- Sadaka hutolewa
- Sadaka inaonesha Upendo
- Tunapotoa sadaka tunakubali kwamba YESU ni dhabihu kamili iliyotolewa msalabani kwa ajili yangu.

**SADAKA INAYOKUBALIKA**

- Ni ile inayotolewa kwa siri kati ya mtu na MUNGU wake
- Ni ile inayotolewa kwa hiari. Kutoka 25:1

**SADAKA ISIYOKUBALIKA**

- Sadaka isyokubalika ni ile inayotolewa kwa wito
- Ni ile inayotolewa kwa shinikizo

- Inayotolewa kwa kujionesha. Luka 18:10-12, Marko 12: 41
- Ni ile inayotolewa ili kukumbukwa.

**KANUNI ZA UTENDAJI KAZI**

1. Ratiba: Kuwa na ratiba ya kazi kuanzia siku inapoanza hadi muda wa kulala
2. Kuwa utaratibu au mpangilio wa kazi/ kazi ifanyike kwa utaratibu
3. Kuwa na malengo yaani kufanya kazi kwa malengo ni sa kwa mazoea
4. Kazi zifanywe kwa kuzingatia muda wa kuanza na kumaliza. Wagalatia 4:4
5. Kufanya kazi kwa mipango. Weka mipango inayoeleweka, weka utaratibu wa kuandika mipango yako. KWa kazi za kanisa unda kamati ya mipango
6. Kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuleta mafanikio
7. Fanya tathmini ya kazi, ili kupata matokeo hasi au chanya.Mwanzo 1:31
    - Kumbuka kazi bila taarifa ni sawa na kutabasamu gizani
8. Kazi ifanyike kwa uzuri. 1Wakorintho 14: 40

**KANUNI 12 ZA UWAKILI**

1. Bwana MUNGU ni mwenye mamlaka na Mtawala. Marko 12: 29, Wafilipi 4: 19. Ni kwa sababu aliumba vitu vyoote
2. Bwana ni Mmiliki. Anamiliki na kuruzuku viumbe vyake. Zaburi 24: 1, 50: 9-15, Walawi 25: 23-24, 1Nyakati 29:14
3. Mungu ni wa kwanza na wa mwisho. Ni mwanzo na asili ya kila kitu, na mwisho wa vyote. Mathayo 6: 34. Chochote kinachochukua nafasi ya MUNGU ni sanamu. Kutoka 20: 3
4. Uwepo wa Bwana katika maisha yetu. Mathayo 28: 20
5. Mwanadamu ni msafri na mpitaji katika dunia hii. Wakolosai 3:2. 1Yohana 2:15
6. Mwanadamu ni mdeni. Ninalo deni ninalodaiwa naye. Yeye alilipa. Yohana 3:16, Warumi 1: 14-16

7. Mtizamo wa furaha. 2Wakorintho 8:12
8. Mikono iliyowazi. Mithali 11: 24-25
9. Koleo kubwa/ moyo wa shukrani na upendo. Zaburi 116:12, 1Wathesalonike 5:18
10. Kanuni ya kuzidisha. Mungu huzidisha tunapotii. 1Wafalme 17:10-16, Mathayo 14:17,20, 15:34, 37
    - Mungu hufanya kazi kwa kuzidisha. Mfano Talanta 5 huwa 10. Mathayo 25: 20 – 25
11. Kanuni ya kuwa na njozi.
    - Kuwa na imani. Waebrania 11:27
    - Kubali kutumika Mathayo 20: 28
12. Kanuni ya ushirika
    - Ushirika pamoja na YESU ni ushindi. Wafilipi 4:13, 1Timotheo 1:12, Waefeso 3:19,20

**RATIBA NA UMUHIMU WAKE**

- Ratiba ni mpangilio wa shughuli apangao mtu au watu huweka katika kufanikisha malengo kwa wakati unaofaa.
- Ratiba ni mwongozo katika kutekeleza majukumu ya kila siku na ya muda mrefu kulingana na muda unaopangwa
- Ni mpango unaoonesha matukio kwa muda uliopangwa.

Mfano: Kuwasili kwa meli, treni au basi. Shuleni au vyuoni, mashambani na kazini lazima kuwepo na ratiba.

**UMUHIMU WA RATIBA**

Ratiba inatusaidia nini?

1. Kujua mambo muhimu, kuyapanga na jinsi ya kuyatekeleza kwa wakati
2. Husaidia kutekeleza wajibu na kufikia malengo
3. Husaidia kufanya kazi kwa wakati
4. Kuwa na matumizi sahihi ya muda

5. Husaidia na kuwezesha kutathmini utekelezaji wa majukumu
6. Huonesha mtiririko wa shughuli/ kazi
7. Hukumbusha wajibu na kuweka nafasi ya uwajibikaji
8. Husaidia viongozi kusimamia, kuhimiza na kufuatilia utekelezaji
9. Husaidia kuokoa mali, muda na rasilimali zako, za kanisa au taasisi husika
10. Huondoa tatizo la mlundikano wa kazi. Mfano wengi huandaa Sabato siku ya Ijumaa na hivyo hujikuta sabato inaingia wangali kazini, na husinzia kwenye Ibada sababu ya uchovu
11. Huondoa Uvivu na kutopenda kufanya kazi

**NYANJA KUU ZA UWAKILI**

**1. UWAKILI WA MWILI**

Warumi 12:1, 1Wakorintho 3:16 -17, 6:19-20

- Miili tuliyonayo ni mali ya MUNGU kwa sababu ndiye Muumbaji
- Alikuja kutukomboa katika dhambi
- Kumchagua bwana mwingine tofauti na BABA wa Mbinguni ni kutafuta hasara kubwa
- Mungu aliweka kanuni za afya kwa ajili ya utanzaji wa miili yetu
    - Amri ama sheria kumi za MUNGU
    - Sheria za asili/ kanuni 8 za afya
        1. Lishe bora
        2. Mazoezi
        3. Maji safi na salama
        4. Mwanga wa jua
        5. Kiasi
        6. Hewa safi
        7. Kupumzika/Pumziko
        8. Imani – kumtumaini na kumtegemea MUNGU

- Mwili unatakiwa kutunzwa kwa kanuni zote nane ikiwa ni pamoja na kufua nguo zote, kuoga, kula na kunywa, usafi wa nyumba n.k

2. **UWAKILI WA WAKATI.** 1Petro 1:17
    - Muda ni zawadi tuliyopewa na MUNGU
    - Wakati/muda tuliopewa tutaoa hesabu ya matumizi yake
    - Muda unapaswa kufanyiwa bajeti.tia 4:4
    - Fanya mambo au kazi kwa wakati. Wagala

**Muda umegawanyika katika sehemu kuu tatu**

1. **Saa 8 za kufanya kazi kwa bidii/juhudi**: 2Wathesalonike 3: 12, 1Wathesalonike 4: 11-12, Mhubiri 9:10
    - Anza kazi na BWANA, kuomba ulinzi na uongozi wake, kwa kusoma Neno na Maombi. 1Wakorintho 10:31
    - Kazi ni agizo la MUNGU, ni lazima kufanya kazi kulingana na utaratibu ili kupata mahitaji yetu, kwa ajili Bwana na kuwagawia wahitaji
2. **Saa 8 za Mambo mbalimbali**
    - Muda huu ni wa kujifunza na kujilisha neon la MUNGU kupitia Biblia, Roho ya Unabii
    - Kuhudhuria vipindi mbalimbali vya ibada na mikutano. Mfano, Vijana kwaya, dorkasi baraza la Kanisa
    - Ni muda wa kushuhudia, mazoezi, kutembeleana n.k
3. **Saa 8 za kupumzika**
    - Mungu ametoa zaidi ya robo ya umri wa mwanadamu kwa ajili ya kupumzika yaani miaka 23
    - Tunapaswa kulala saa 8
    - Usingizi ni muhimu sana. Unapokosa usingizi mwili hudhoofika jambo ambalo husababisha utendaji mbovu wa kazi. (uzembe na uvivu
    - Hata kama huna usingizi pumzika tu kitandani.

**Wezi wakubwa wa Muda:**

1. Uzururaji wa holela/ ovyo bila kuwa na kusudi mkimaishaalumu wala kwa faida ya maisha

2. Michezo hafifu kama bao,draft, vijiwe vya kahawa,na vijiwe vya hadithi zisizojenga. Zaburi 1:1-5, 1 Timotheo 4:7…
3. Kukaa muda mrefu kuangalia Tv, matumizi ya mtandao (internet), simu, bila kuwa na kiasi.
4. Kufanya kazi bila ratiba ama mpangilio wa kazi
5. Kulala kupita kiasi. Ni chanzo cha uvivu na umaskini. Mithali 6: 9-11, Mithali 22:13, 26:13
6. Kuahirisha kazi bila sababu ya msingi.
7. Kufanya kazi bila kuzingatia kanuni
8. Matumizi yasiyofaa ya saa Takatifu za Sabato

**3.UWAKILI WA TALANTA**

Mathayo 25:14-25, Luka 19: 12-27, Waefeso 4:8, 1Wakorintho 12:8

Talanta- Ni uwezo Mungu atowao kuwa mtu tangu kuzaliwa mfano; kuimba, kuchora, kuhubiri n.k

Talanta huongezeka zinapotumika, na hupungua ama kufa zisipotumika.

Karama- Uwezo wa MUNGU apewao mwanadamu kwa wakati kwa kusudi fulani mfano unabii

**4.UWAKILI WA MALI. Zaburi 24:1**

- Mali ni zao la wakati na talanta
- Mali hupatikana kwa kufanya kazi kwa kutumia vizuri muda na talanta
- Mali yaweza kuwa fedha, shamba, nyumba, mifugo, n,k
- Mali tulizonazo tumepewa na MUNGU kama mawakili tu. 1Wakorintho 4:1
- Mali tunazopewa ni za MUNGU ambazo tunapaswa kurudisha na kuleta kwake.

**5.UWAKILI WA MIVUTO YETU**: Warumi 14:20-21

- Kila mkristo anao wajibu wa kuwajibika kwa kile tunachosema na kuamini, utendaji wa siku kwa siku.
- Mwonekano wetu uwe ule unaoaksi tabia ya Kristo na ionekane kwa watu na kuwavuta kwa YESU kwa kadiri ya imani yetu.

**6.UWAKILI WA KUJALI:** Mathayo 25: 45

- Kila mmoja anapaswa kujali watu wote ambao Kristo alikufa kwa ajili yao
- Kujali ni dini iliyo safi mbele za MUNGU BABA na ndio utimilifu wa sheria ya Upendo. Yakobo 1:27, Mathayo 22:37-40, Mathayo 25:45…